

WE ARE YOUR DOL



Department
of Labor



KITENGO CHA UZINGATIAJI NA ELIMU

KITENGO CHA UZINGATIAJI NA ELIMU (DOCE)

Kitengo cha Uzingatiaji na Elimu (DOCE) (kilichokuwa kikijulikana kama Kitengo cha Sera na Masuala ya Wahamiaji) huhakikisha kuwa huduma, mipango na ulinzi wa Idara ya Leba zinapatikana kwa wafanyakazi wote. Hii inajumuisha vikundi vinavyokua vya watu waliohamia katika Jimbo la New York kutoka nchi zingine na wale wanaozungumza lugha zingine kando na Kiingereza.

UHAMASISHAJI

DOCE huwajulisha wahamiaji, wakimbizi, na Wanafunzi wa Lugha ya Kiingereza kuhusu haki zao kazini. Tunawaeleza kuhusu usaidizi unaotolewa na Idara ya Leba ya Jimbo la New York (NYS DOL), kama vile:

- Hatua za kuchukuliwa kuhusu mishahara ambayo haijalipwa, saa ya ziada na manufaa mengine
- Ukweli kuhusu bima ya ukosefu wa ajira
- Msaada wa kutafuta kazi na usaidizi wa kikazi
- Viungo vya kufikia mashirika na vikundi vingine kwa ajili ya usaidizi
- Maelezo kuhusu Usafirishaji Haramu wa Binadamu

DOCE pia inawaelimisha wamiliki wa biashara ndogo kuhusu:

- Sheria za ajira
- Majukumu yao ya kisheria
- Rasilmali za Idara ya Leba ambazo zinaweza kuwasaidia
- Usafirishaji Haramu wa Binadamu

SERA NA SHERIA

DOCE inafanya kazi ili kuhakikisha kuwa Idara ya Leba ya Jimbo la New York inakidhi mahitaji ya wahamiaji, wakimbizi na Wanafunzi wa Lugha ya Kiingereza. Tunakagua jinsi sera, taratibu na sheria za NYSDOL zinavyoathiri jamii zao.

WAATHIRIWA WA UHALIFU

Usafirishaji Haramu wa Binadamu na kazi ya kulazimishwa ni uhalifu unaowakandamiza wakazi wa New York, wakiwemo wahamiaji, wakimbizi na Wanafunzi wa Lugha ya Kiingereza. DOCE husaidia kupambana nao jimboni kote. Pia tunawaelekeza waathiriwa kwa mashirika ya jimbo ambayo yanaweza kuwasaidia kupata huduma wanzostahili kupata chini ya sheria za makosa ya jinai za jimbo.

Waathiriwa wa uhalifu fulani wanaweza kutuma maombi kwa serikali kuu kwa ajili ya kupewa visa maalum Ili kutuma maombi, ni sharti waidhinishwe kupitia taasisi za kutekeleza sheria. Ndani ya Idara ya Leba, DOCE hukagua maombi ya uidhinishaji wa viza za U na T.

KILIMO

DOCE inajitahidi kuimarisha sekta kubwa na anuwai ya kilimo ya New York. Pia, tunawaelimisha wafanyakazi wa kilimo kuhusu haki zao na huduma zinazopatikana kupitia Idara ya Leba. Tunatembelea mashamba ili kuwasaidia waajiri kuzingatia sheria za kazi. Pia tunasaidia wakulima kupata wafanyakazi wa kilimo waliohitimu ili kukidhi mahitaji yao ya kazi. DOCE hushughulikia maombi ya H-2A, hufanya ukaguzi wa nyumba, hutoa usaidizi wa mahojiano ya lugha ya Kihispania, na hufanya kazi ili kusaidia Idara ya Leba ya Marekani katika kuhakikisha kuwa mikataba ya H-2A inatii sheria.

WASILIANA NA DOCE

Nambari ya simu: **877-466-9757 (877- IMM-WRKR)**

Barua pepe: **doce@labor.ny.gov**

Tovuti: **www.labor.ny.gov**